



TAASISI YA UTAFITI WA WANYAMAPORI TANZANIA (TAWIRI)

Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, **“Tanzania Wildlife Research Institute” (TAWIRI)** ni Taasisi ya Umma chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 4 ya mwaka 1980. Awali Taasisi hii ilijulikana kama Taasisi ya utafiti wa wanyamapori Serengeti **“Serengeti Wildlife Research Institute” (SWRI)** na mwaka 1999 ilibadilishwa jina kuwa TAWIRI ili kukidhi sura ya kitaifa kwa Sheria ya Bunge Na. 10 ya 1999 (Sura 260, Toleo la 2002). Kwa kifupi utafiti wa wanyamapori nchini ulianza miaka ya 1950, na kwa mara ya kwanza, mwaka 1963 Taasisi ya utafiti iliyojulikana kama “Serengeti Research Institute” (SRI) ilianza kusimamia utafiti huu chini ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) hadi mwaka 1980 jukumu hili lilipokabidhiwa rasmi TAWIRI.

Dira ya TAWIRI ni kufikia kiwango cha juu cha utafiti ili kuweza kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakati muafaka kuhusu uhifadhi endelevu wa wanyamapori nchini.

Dhamira kuu, ni kuendesha na kusimamia utafiti wa wanyamapori nchini, kutoa takwimu na ushauri wa kitaalamu ili kuiwezesha Serikali na wadau husika katika kusimamia uhifadhi endelevu wa wanyamapori katika nchi yetu.

Majukumu ya Taasisi ni kufanya, kusimamia na kuratibu tafiti za wanyamapori nchini, kuwezesha Watanzania kupata nafasi za mafunzo na elimu, kushirikiana na taasisi mbalimbali zilizo ndani na nje ya nchi kufanya tafiti, kusambaza taarifa na kutuoia elimu kwa umma kupitia matokeo ya tafiti mbalimbali za wanyamapori. Vilevile Taasisi ina jukumu kubwa la kuishauri Serikali, mamlaka za usimamizi wa wanyamapori na Watanzania kwa ujumla kuhusu uhifadhi endelevu wa rasilimali kama ilivyoelekezwa katika *Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori ya mwaka 1980*.

TAWIRI imeendelea kutekeleza shughuli za utafiti wa wanyamapori kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Taasisi za uhifadhi wa wanyamapori na wadau wote wa uhifadhi. Kwa kupitia tafiti mbalimbali, Taasisi imechangia kutoa ushauri wa kina kwa Serikali na wadau mfano, mbinu bora za kupunguza migogoro baina ya wananchi na wanyamapori, namna ya kuzuia magonjwa mtambuka kutoka wanyamapori-mifugo-binadamu, hali ya mwenendo wa wanyamapori nchini, tathmini ya mapito ya

wanyamapori, uandaaji mipango mkakati ya kuhifadhi wanyama adimu mfano, faru, sokwemtu, tembo, twiga, na tafiti nyingine kama inavyoelekezwa na Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwa kutambua umuhimu wa jukumu la Kitaifa linalotekelezwa na TAWIRI, Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Khamis Kigwangalla (Mb), kwa nyakati tofauti amekuwa akiunga mkono juhudi za TAWIRI na kuwasahi wadau wa uhifadhi kuunga mkono juhudi hizi ili kusaidia uhifadhi wa wanyamapori nchini.

“Natambua kazi nzuri za tafiti zinazofanywa na TAWIRI na wadau wa tafiti za wanyamapori nchini. Ili kukidhi malengo ya uhifadhi na maendeleo ya jamii, taarifa za uhakika za kisayansi zinahitajika ili kuwezesha watunga sera na wasimamizi wa utekelezaji wa sera, sheria na miongozo ya uhifadhi kuweka vipaumbele ili kufikia malengo husika. Nawasahi watafiti wote kuwa mstari wa mbele kufanya tafiti zenye tija kwa Taifa letu. Pia Mamlaka za uhifadhi na wadau wa uhifadhi tumieni matokeo haya kutekeleza shughuli mbalimbali kwa uhifadhi endelevu wa maliasili zetu na kuboresha maisha ya jamii”. Mheshimiwa Waziri aliyasema haya tarehe 4/12/2019 alipokuwa akikabidhi tuzo za heshima kwa watafiti na taasisi ambazo zimekuwa mstari wa mbele kusaidia shughuli za utafiti wa wanyamapori nchini, katika Kongamano la 12 la TAWIRI la Kisanyansi lililokutanisha washiriki zaidi ya 300 kutoka mataifa 16 duniani, ambalo lilifanyika Mkoani Arusha tarehe 4-6 Disemba 2019.

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:

Tovuti: www.tawiri.or.tz:

Barua pepe: info@tawiri.or.tz:

Simu: +255 27 254 9571